**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents Government Budget Speeches

2005-07

# Hotuba ya Waziri wa Fedha Mh.Basil P.Mramba (Mb) akiwasilisha bungeni kuhusu mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2005-2006

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/680

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

INFORMATION AND RESEACH UNIT
GOVT PRESS—DSM

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA MHESHIMIWA BASIL P. MRAMBA (MB.), AKIWASILISHA KATIKA BUNGE MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2005/2006






KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA MKUU WA SERIKALI, DAR ES SALAAM - TANZANIA

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA MHESHIMIWA BASIL P. MRAMBA (MB.), AKIWASILISHA KATIKA BUNGE MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2005/06

## UTANGULIZI:

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, Bunge likubali kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2005/06. Pamoja na hotuba hii, kuna vitabu vinne vinavyoelezea kwa undani bajeti hii. Kitabu cha kwanza kinaelezea makadirio ya mapato, cha pili kinahusu makisio ya matumizi ya kawaida kwa Wizara na Idara, kitabu cha tatu kinahusu matumizi ya Halmashauri za Miji na Wilaya, Kitabu cha nne ni cha makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara, Idara, Mikoa na Halmashauri. Kadhalika, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2005/06.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya bajeti hii. Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge lako tukufu, pamoja na Kamati nyingine za Kisekta, zilifanya kazi nzuri sana kuchambua makisio haya kwa kina na kutoa ushauri ambao umezingatiwa katika

bajeti hii. Aidha, napenda kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha Miswada na nyaraka mbalimbali za Sheria ambazo ni sehemu ya bajeti hii. Napenda pia kuwashukuru wafanyakazi wenzangu wote wa Wizara ya Fedha, hususani Manaibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Alhaj Abdisalaam Issa Khatibu (Mb.) na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu (Mb.); Makatibu Wakuu, Bw. Gray S. Mgonja na Bw. Peniel M. Lyimo; Naibu Katibu Mkuu, Bw. Ramadhani M. Khijjah; Wakuu wa Idara, na wafanyakazi wote, kwa kufanikisha maandalizi ya bajeti hii. Pia, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ambaye ameweza kuchapisha kwa wakati hotuba hii, vitabu vya bajeti na nyaraka nyingine kwa ufanisi mkubwa. Nawashukuru wale wote waliowasilisha kwangu mapendekezo mbalimbali kuhusu kodi, na kuhusu Sera za Mapato na Matumizi kwa ujumla. Ushauri wao umechangia kwa kiwango kikubwa katika kukamilisha bajeti hii.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** katika miezi kumi na moja iliyopita, tumepoteza Wabunge wenzetu watano ambao waliaga dunia. Wabunge hao ni: Hayati Mheshimiwa Yete Simtemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Hayati Mheshimiwa Theodos James Kasapila, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Hayati Mheshimiwa Frank Michael Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Hayati

Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo na Hayati Mheshimiwa Abubakar Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu hawa mahali pema peponi, Amina.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** hiki ni kikao cha mwisho cha bajeti kwa Bunge hili la Awamu ya Tatu. Bajeti ya leo ni ya kumi tangu Serikali ya Awamu ya Tatu iingie madarakani mwezi Novemba 1995. Wengi wetu tunarudi kwa wananchi kwa mujibu wa sheria na taratibu, kuomba ridhaa yao ya kurudi tena katika ukumbi huu ambao utakuwa mpya. Nina matumaini makubwa sana kuwa wananchi hawatasahau mema na makubwa mengi yaliyofanywa na Bunge la awamu ya tatu na Serikali yake. Awamu ya Tatu chini ya uongozi wa Rais Benjamin William Mkapa imepata mafanikio makubwa na ya kujivunia, hasa katika kufufua na kukuza uchumi, kuimarisha miundombinu na kutoa huduma kadhaa za jamii. Uwezo wa Serikali wa kutoa huduma za msingi za uchumi na za jamii **umeongezeka zaidi ya mara tatu** katika kipindi cha miaka tisa ya utawala wa Awamu ya Tatu.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulipongeza Bunge lako tukufu chini ya Uongozi wako, kwa mchango mkubwa ambao umeiwezesha Serikali

ya CCM ya Awamu ya Tatu kufikia mafanikio makubwa. Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza mwenzetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa CCM Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa na CCM, kwa kura nyingi, kugombea nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM. Chaguo hilo la CCM ni alama ya imani ya Chama hicho kwetu sisi Wabunge na Bunge lenyewe kama taasisi, na ni mfano unaostahili kuigwa na Vyama vyote vya siasa nchini.

6. ***Mheshimiwa Spika***, kama nilivyosema awali, bajeti hii ni ya kumi tangu Serikali ya Awamu ya Tatu iingie madarakani mwezi Novemba, 1995. Katika kipindi hicho, Bajeti ya Serikali imekuwa chombo muhimu cha kusukuma maendeleo ya nchi. Kwa kuweka misingi imara ya usimamizi wa bajeti, hali ya uchumi kwa ujumla imekuwa tulivu, kwa sababu tumejifunza kutumia kile tulichonacho.

## TULIKOTOKA NA TUNAKOKWENDA

### (A) MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA TATU

7. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha miaka tisa iliyopita, Tanzania imepata mafanikio makubwa, licha ya vikwazo vingi kama vile

mafuriko ya mvua za Elnino, ukame, kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli katika soko la nje, kushuka kwa bei ya mazao ya kilimo katika soko la dunia, na mambo mengine mengi. Licha ya vikwazo hivi, Serikali ya Awamu ya Tatu imefanya mambo makubwa kwa lengo la kufanya maisha ya Watanzania yawe bora na salama. Baadhi ya mafanikio hayo ameyaeleza vizuri Mheshimiwa Abdalah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Mengine yataelezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wa kisekta watakapo wasilisha hoja zao.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa msisitizo, mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu ni pamoja na haya yafuatayo:

(a) Kuweka misingi imara ya kukusanya mapato ya ndani, na kwa kuwa na ushirikiano mzuri na wafadhili, na kusimamia bajeti ya Serikali kwa ufasaha. Serikali imejenga uchumi tulivu.

(b) Kujenga nidhamu ya kutumia tulicho nacho bila kuchapisha noti ovyo. Tumeweza kushusha mfumuko wa bei kutoka asilimia 21 mwaka 1996 hadi kufikia asilimia 4 mwaka 2005.

(c) Kasi ya kukua kwa Pato la Taifa imeongezeka kutoka asilimia 4.2 mwaka 1996 hadi asilimia 6.7 mwaka 2004. Kasi hii ya kukua kwa uchumi inaiweka Tanzania kileleni miongoni mwa nchi nyingi za Afrika.

(d) Urari wa malipo ya nje umeimarika kwa kiwango kikubwa. Akiba ya fedha za kigeni sasa inatosha kununua bidhaa na huduma kutoka nje kwa mahitaji ya miezi 7, kulinganisha na miezi miwili miaka kumi iliyopita. Ingawa mauzo yetu katika soko la kimataifa hayajaongezeka kwa kiwango kikubwa, urari wa malipo ya nje umekuwa mzuri kwa sababu ya uwekezaji, misaada ya nje ambayo imeongezeka zaidi ya mara tatu, ikiwemo misamaha ya madeni, kukua kwa utalii, na matokeo ya sera ya kuruhusu biashara huria ya fedha za kigeni.

(e) Kwa kuvutiwa na mazingira mazuri ya uwekezaji, sasa ziko benki za biashara 26 badala ya 2 tu zilizokuwepo mwaka 1996. Aidha, ziko taasisi nyingine tano za fedha sasa badala ya mbili tu zilizokuwepo mwaka 1996. Mikopo ya benki imeongezeka na sasa inakua kwa kiwango cha asilimia 30 kwa

mwaka. Riba ya mikopo imeshuka kwa wastani kutoka asilimia 26 mwaka 1996 hadi asilimia 14.4 mwaka 2004.

(f) Masoko ya fedha yamekua. Sasa liko soko la hisa, ziko kampuni za bima karibu kumi, na vyombo vingine vingi ambavyo havikuwepo miaka kumi iliyopita.

9. ***Mheshimiwa Spika***, nguzo kuu ya uchumi endelevu ni akiba ya ndani ya nchi inayoambatana na uwekezaji. Akiba ya ndani inakusanywa kupitia njia mbili kuu, ambazo ni kodi na amana za wananchi na wafanyabiashara wanazowekeza katika vyombo vya fedha. Kodi ndio chanzo kikuu kinachoipa Serikali uwezo wa kuendeleza huduma za uchumi, huduma za jamii, ulinzi na usalama, pamoja na uwekezaji katika miradi ya maendeleo.

10. ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 1995/96 Serikali ilikusanya shilingi bilioni 448.4 kwa mwaka au shilingi bilion 37 kwa mwezi. Mwaka huu wa 2004/05, Serikali inakusanya shilingi trilioni 1.774, sawa na shilingi bilioni 145 kwa mwezi. Hili ni ongezeko la zaidi ya mara nne katika kipindi cha miaka kumi.

11. ***Mheshimiwa Spika***, ongezeko la ukusanyaji wa mapato limetokana na sera thabiti zilizotekelezwa katika kipindi hicho. Kwa muhtasari, mambo yafuatayo yalitekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tatu:-

(a) Sera za kodi na mfumo wake zilifanyiwa mageuzi makubwa, ambayo ni pamoja na kuwianisha na kuhuisha kodi mbalimbali kwa lengo la kurahisisha ukusanyaji wake.

(b) Idadi kubwa ya kodi zenye tija ndogo au zenye kero kwa wananchi zilifutwa ikiwemo kodi ya maendeleo.

(c) Kodi mpya ya Ongezeko la Thamani (VAT) ilianzishwa mwaka 1997.

(d) Mianya ya kukwepa kodi, hasa ushuru wa forodha imezibwa kwa kiwango kikubwa.

(e) Usimamizi wa ukusanyaji mapato chini ya Mamlaka ya Mapato (TRA) umeimarishwa kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano, sasa kuna Idara ya Walipa Kodi Wakubwa ambao wanasikilizwa kwa umakini mkubwa, jambo ambalo linaongeza ari ya wao kulipa kodi bila kusukumwa mno.

(f) Serikali imeanzisha utaratibu wa kujadiliana na walipa kodi kila

mwaka kuhusu sera na viwango vya kodi. Utaratibu huu pia umesaidia kuongeza utiifu katika kulipa kodi kwa hiari.

(g) Sheria mbalimbali za kodi zimetungwa upya au zimerekebishwa, ili ziende na wakati.

(h) Utawala wa Mamlaka ya Mapato Tanzania umeimarishwa kwa kiwango kikubwa, na bado unaendelea kuimarishwa.

(i) Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi zilianzishwa mwaka 2000 kwa lengo la kusikiliza malalamiko ya walipa kodi.

(j) Taratibu za forodha zimeboreshwa na kuwa za kisasa. Kwa mfano mafuta ya petroli yanapoingizwa nchini kupitia Dar es Salaam yanapita kwenye kipimo maalum kinachojulikana kama "Flow Meter". Aidha, mizigo inayokuja kwenye makontena sasa inachujwa na mashine maalum inayoitwa "Container Scanner" ili kudhibiti ukwepaji kodi.

12. ***Mheshimiwa Spika***, hatua hizi pamoja na nyingine, ndizo zinazoiwezesha Serikali

kuongeza ukusanyaji wa mapato **zaidi ya mara nne katika kipindi hicho.** Ukusanyaji mzuri wa mapato ya ndani, pamoja na misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka kwa Nchi Marafiki na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa, viliiwezesha Serikali kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika programu za **Afya, Elimu, Barabara, Maji, Kilimo,** na sekta nyinginezo. Katika kipindi hicho, **mgao wa fedha za bajeti kwa ajili ya sekta hizo uliongezeka karibu mara nne,** na matokeo ya hatua hizi yanaonekana katika sekta hizo.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na sera sahihi za uchumi, utawala bora, na uwajibikaji, ikiwepo nidhamu ya matumizi ya mali ya umma, tumerejesha uhusiano mzuri wa misingi ya ushirikiano (partnership) na wafadhili wetu, na hivyo **misaada ya nje imeongezeka zaidi ya mara tatu katika miaka kumi iliyopita.** Misaada ya nje na mikopo ya masharti nafuu imeongezeka kutoka shilingi bilioni 187 mwaka 1995/96 hadi shilingi trilioni 1.7 mwaka huu. Aidha, mkakati wa Serikali ya Tanzania wa kusimamia misaada umechangia katika ongezeko la misaada hasa ile inayopitia kwenye bajeti yetu. **Awamu hii ilipoingia madarakani, hakukuwa na misaada ya bajeti.** Misaada yote ilikuwa ikitolewa kwa njia ya miradi, ambayo kwa kiasi kikubwa ilikua inabuniwa na kusimamiwa na wafadhili wenyewe. Serikali

haikuwa na uelewa wa mambo yanayotokea huko kwenye miradi. Utaratibu huo sasa umebadilika. **Sisi wenyewe ndio tunabuni miradi na kusimamia utekelezaji wake. Sehemu kubwa ya misaada sasa inatolewa kupitia Bajeti ya Serikali (Budget Support). Hata Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika, zinatoa sehemu kubwa ya mikopo ya masharti nafuu kupitia Bajeti ya Serikali. Huu ni ushahidi tosha kwamba dunia ina imani na Serikali ya Mkapa** kwani hili wanalifanya kwa nchi chache sana Afrika Kusini mwa Sahara.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na sera sahihi za uchumi, imani ya Nchi Marafiki na Mashirika Wafadhili kwa Serikali ya Tanzania imetokana pia na mageuzi tuliyofanya katika usimamizi wa fedha na uwajibikaji wa Serikali. Uamuzi wa kuwekeza katika mfumo wa mtandao wa malipo Serikalini (IFMS), na mpango unaoendelea wa mageuzi ya usimamizi wa fedha za umma vimekuwa vichocheo muhimu vya sisi kuaminiwa na hao wanaotusaidia, kwa imani kwamba misaada yao itatumiwa kwa malengo tuliyokubaliana nao. Ushirikiano huu mzuri kati ya Tanzania na Wafadhili umekuwa unasimamiwa chini ya utaratibu ujulikanao kama "Mkakati wa Tanzania wa Kusimamia Misaada," "Tanzania Assistance Strategy," ambao sasa unaimarishwa

zaidi na utakuwa unaitwa 'Mkakati wa Pamoja wa Kusimamia Misaada' (Joint Assistance Strategy - JAS).

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Tatu imeweka juhudi kubwa kushughulikia tatizo tulilokuwa nalo la mzigo wa madeni. Nchi yetu ilikuwa na limbikizo kubwa la deni ambalo halikuwa rahisi kulilipa kwa kuwa mapato yetu yalikuwa kidogo sana. Kwa maana hiyo, **Tanzania ilikuwa haikopesheki tena**. Ili kurejesha heshima ya Nchi, Serikali hii iliamua kujikokota kulipa baadhi ya madeni kidogo kidogo. Papo hapo Serikali iliungana na wadau wengine wa kimataifa kutaka Nchi na Mashirika tajiri zifute madeni ya nchi maskini kama Tanzania. Serikali pia ilibuni sera na mkakati mpya wa kitaifa wa kusimamia madeni. Katika kipindi hicho, walikuwepo baadhi ya watu waliohoji mantiki ya kulipa madeni wakati uchumi wetu ulikuwa dhaifu.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** mkakati huo wa Serikali wa kulipa madeni ulizaa matunda pale Tanzania ilipoingizwa kwenye kundi la nchi masikini zenye madeni makubwa sana duniani "HIPC" ambazo zilistahili kufutiwa sehemu kubwa ya madeni yao. Matokeo yake ni kwamba **Tanzania imesamehewa madeni kiasi cha shilingi trilioni tatu** yatakayoiva katika kipindi cha miaka ishirini ijayo. **Hadi sasa**

**tumeshafutiwa madeni yenye thamani ya takriban shilingi trilioni 1.3. Hadhi ya Tanzania kimataifa imepanda, na sasa nchi inakoposheka tena, kwa kuwa inao uwezo wa kulipa madeni** yake. Sisi **leo tunachagua wapi tukakope,** kinyume na miaka ya nyuma ambapo tulikuwa hatukopesheki. Hata hivyo, tunatambua kwamba bado tuna madeni ya kulipa na kwa kuwa nchi yetu ni changa, shinikizo la kutaka kufutiwa madeni yaliyobaki bado linaendelea.

17. ***Mheshimiwa Spika***, jitihada za Serikali hazikuishia kwenye kusafisha taswira yake kwa nchi na taasisi za nje zinazotudai. Katika kipindi cha 1995/96 hadi 2003/04, madeni ya ndani yaliyofikia shilingi bilioni 144.3 yamehakikiwa na kulipwa. Kiasi hiki kinajumuisha fidia ya shilingi bilioni 12.3, madeni ya wazabuni shilingi bilioni 111, na limbikizo la mishahara ya watumishi wa Serikali, kama vile walimu shilingi bilioni 21. Hatua hii ilisaidia kuzindua sekta binafsi ya ndani ambayo ilikuwa imeathirika kutokana na kucheleweshewa malipo yao. Aidha, madeni mengine ya ndani yakiwemo ya fidia mbalimbali yanaendelea kuchambuliwa na kuhakikiwa.

**Uwezeshaji wa Wananchi**

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho cha miaka 10 cha Serikali ya Awamu ya Tatu,

hatua nyingi za kuwawezesha wananchi kumiliki uchumi wao na kujiletea maendeleo yao zimetekelezwa, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imetunga Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi, na Bunge limetunga Sheria ya kutekeleza Sera hiyo, na hivi sasa imeanza kutekelezwa.

(b) Serikali ilibuni na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambao unawashirikisha kwa karibu sana wananchi kupitia Serikali za Vijiji katika kubuni na kupanga miradi ya maendeleo, Mradi huu umekuwa na mafanikio makubwa sana. Hivi majuzi, Awamu ya Pili yenye bajeti ya takriban shilingi 180 bilioni imezinduliwa na Mheshimiwa Rais kitaifa Wilayani Magu.

(c) Aidha, Serikali imebuni, inatafiti, na inatekeleza programu maalum ya kurasimisha raslimali za sekta isiyo rasmi ili kuwawezesha wananchi kutumia raslimali zao kama dhamana ya kukopa kutoka benki.

(d) Kama nilivyosema awali, Serikali imebuni Sera ya Taifa ya Mikopo Midogo Midogo (*National Micro*

*Finance Policy*) ya mwaka 2001. Taratibu na Kanuni za utekelezaji wa sera hiyo zimekamilika na kuchapishwa. Wananchi wengi wa kipato cha chini wanategemewa kufaidika na mpango huu.

(e) Serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu imeanzisha Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya benki kwa ajili ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi (*Export Credit Guarantee Scheme-ECGS*). Mfuko huu unasaidia sana hasa vyama vya ushirika kununua mazao ya biashara kwa wakulima na kuuza nje ya nchi. Wawekezaji katika maeneo maalum ya kuzalisha na kuuza nje (EPZ) pia wanafaidika na Mfuko huu.

(f) Serikali pia imeanzisha Mfuko wa kudhamini mikopo ya benki kwa wawekezaji wadogo na wa kati, ambapo kiasi cha Shilingi 2.0 bilioni zimekwishatolewa hadi sasa. Aidha, Serikali iko karibu kukamilisha uanzishwaji wa Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya muda mrefu.

(g) Serikali imetekeleza mageuzi makubwa katika sekta ya mabenki na taasisi za fedha

nchini ambayo yatawanufaisha sana wateja.

(h) Pamoja na mageuzi hayo, zoezi la kuirekebisha Benki ya Rasilimali (TIB) ili iweze kuwa benki ya maendeleo sasa liko katika hatua za mwisho. Aidha, zoezi linaendelea pia la kuiwezesha mifuko ya hifadhi ya jamii kutoa mikopo ya muda mrefu na mikopo ya nyumba kupitia benki na vyombo vingine vya fedha.

(i) Wakati huo huo, Serikali inashirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi (HABITAT) kutengeneza mazingira ya kuwezesha kupatikana mikopo ya nyumba.

(j) Serikali inashirikiana pia na Shirika tanzu la Benki ya Dunia (IFC) pamoja na baadhi ya Nchi Wafadhili kujenga mazingira ya kuwezesha ukopeshaji wa vifaa (leasing) hasa vifaa vya uzalishaji. Mpango huu, unaohusisha IFC, Serikali ya Switzerland, na Serikali ya Tanzania, kwa kuanzia, ulizinduliwa mwezi Mei, 2005.

(k) Katika hatua za kuimarisha Benki Kuu ya Tanzania na kuiongezea uwezo wa kusimamia sekta ya

benki, Serikali itawasilisha katika Bunge hili mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 1995, na Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 1991.

(l) Taratibu za utekelezaji wa mabadiliko ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 2004 zitasaidia mikopo mingi kutolewa na mabenki kwa kutambua umilikaji wa ardhi kama dhamana (*collateral*) halali kwa mabenki wakati wa utoaji mikopo.

(m) Kuanzishwa kwa Soko la Hisa la Dar es Salaam (Dar es Salaam Stock Exchange - DSE) pamoja na Mamlaka ya Soko la Mitaji (Capital Markets & Security Authority - CMSA) kunaweka mazingira mazuri ya ushiriki wa wananchi katika kumiliki hisa. Hivi sasa wananchi zaidi ya 67,000 wanamiliki hisa za kampuni mbalimbali zilizoorodheshwa katika soko hilo.

(n) Serikali inatekeleza Mpango wa Kupanua Huduma za Fedha Vijijini (*RFSP*), kwa kuweka kanuni za uendeshaji wa Benki Kata na vyombo vingine vidogo

vya wanachama vya kuweka na kukopa (member-based micro credit entities). Kuanzia sasa vikundi hivyo vitasimamiwa kwa **miongozo itakayotolewa na Benki Kuu ya Tanzania** kitaifa kwa msingi wa sera za Serikali na za uendeshaji bora (best practice) wa taasisi za aina hii. Benki Kuu inategemewa kukasimu madaraka yake kwa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri na Idara zao za Maendeleo ya Jamii, ambao watapewa madaraka ya kuandikisha vikundi hivyo kisheria hapo hapo Wilayani na kuvitekelezea wajibu wa kitaalamu na kiutawala kama itakavyoelekezwa. Hatua hii itaondoa utata uliojitokeza kwa baadhi ya watendaji kutoelewa hali ya vikundi kuwa vya ushirika (SACCOs) chini ya sheria ya ushirika na visivyo ushirika (SACAs) ambavyo sasa taratibu hizi ambazo pia ni za kisheria zitatumika kuviandikisha na kuvihudumia chini ya Mkurugenzi Mtendaji, kwa kutumia Idara zake

za Ushirika kwa SACCOs na Maendeleo ya Jamii kwa SACAs au Benkikata. Ni vema ifahamike kuwa ndani ya Wilaya moja SACCOs na SACAs/Benkikata zinaweza kuungana kuunda **Benkikata** kubwa au **Benki ya Wananchi** iliyo kubwa zaidi.

(o) Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji (Unit Trust of Tanzania – UTT) ambao ulianzishwa mwaka 2003 chini ya Sheria ya Udhamini, umeanza kufanya kazi kikamilifu. Baada ya maandalizi kukamilika, utaratibu wa uwekezaji chini ya UTT kwa jina la Mfuko wa Umoja (Umoja Fund) umeanza tarehe 16 Mei, 2005 ambapo wananchi sasa wana fursa ya kuwekeza kwenye mfuko huo kwa kununua dhamana (units). Ili kufanikisha malengo ya Mfuko, Serikali imefanya yafuatayo kwa dhamira ya uwezeshaji:-

(i) Imetoa asilimia 2 ya hisa zake katika Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) na asilimia 1 katika Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC) kama mtaji wa mwanzo wa Mfuko wa

Umoja. Hisa hizo zina thamani ya shilingi bilioni 10.9.

(ii) Imetoa punguzo la asilimia 30 katika bei ya dhamana (units) za mfuko ili kuwezesha wananchi wengi kumiliki dhamana za Mfuko wa Umoja.

(iii) Dhamana zinauzwa kwa raia wa Tanzania, kampuni zinazomilikiwa na raia, na Mifuko ya Akiba ya Uzeeni ya hapa nchini tu. Benki hazitaruhusiwa kushiriki katika hatua ya mwanzo ya Mfuko.

**Hatua za kuondoa Kero kwa Wananchi**

19. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na hatua hizo nilizoeleza, Serikali pia imetekeleza hatua za makusudi za kupunguza tofauti za mapato katika jamii na kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili wananchi. Hatua hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Ada zote katika shule za msingi zimefutwa ili kuwawezesha watoto wote wenye umri wa kwenda shule kuandikishwa. Aidha, ada katika Shule za Sekondari za kutwa za Serikali zimepunguzwa kutoka

Shilingi 40,000/= hadi shilingi 20,000/= kwa mwaka;

(ii) kodi na ada mbalimbali zinazowaletea kero wananchi, ikiwemo kodi ya maendeleo, zimefutwa;

(iii) Serikali inatoa ruzuku ya usafirishaji wa mbolea kwa manufaa ya wakulima.

(iv) kodi za zana za kilimo zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kama matrekta zimefutwa ili kupunguza gharama za uzalishaji;

(v) Serikali inatoa bure huduma ya tiba katika hospitali na vituo vya afya kwa wanawake wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, wagonjwa wa ukoma, kifua kikuu, na ukimwi.

(vi) mishahara ya watumishi wa Serikali imeongezwa ambapo kima cha chini cha mishahara ya watumishi wa Serikali kimeongezwa kutoka Shilingi 17,500/= kwa mwezi mwaka 1995 hadi Shilingi 60,000/= kwa mwezi mwaka 2004; na

(vii) wastaafu waliolipwa pensheni kwa mtindo wa mkupuo wamerejeshwa katika daftari la pensheni ili kuwasaidia kumudu hali ya maisha. Kima cha chini cha pensheni kimeongezwa pia.

## (B) CHANGAMOTO ZILIZO MBELE YETU

20. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio mengi ya kiuchumi na fedha ya Serikali ya Awamu ya Tatu, nchi yetu bado inakabiliwa na changamoto nyingi, zikiwemo zifuatazo:

(i) Nchi yetu bado ni maskini sana. Tukizingatia kwamba idadi ya watu inaongezeka kwa karibu asilimia 3 kwa mwaka, tunalazimika kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi hadi asilimia 10 kwa mwaka ili tufikie lengo la dira ya Taifa ya kufikia kiwango cha mapato ya kati (Middle Income Country) mwaka 2025. **Ubunifu zaidi, ari mpya na kasi mpya ya kweli vinahitajika ili kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi. Hii ni changamoto kubwa inayolikabili Taifa kwa sasa.**

(ii) Bajeti ya Serikali bado ni tegemezi kwa asilimia 41. Kwa hivyo, tunalo jukumu kubwa la kuongeza zaidi ukusanyaji wa mapato ya ndani. Pamoja na kuimarisha Mamlaka ya Mapato na kuboresha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi, **kasi kubwa zaidi ya kukua kwa uchumi ndio mkakati mkuu utakaofanikisha azma yetu ya kujitegemea.**

(iii) Sehemu kubwa ya mapato yetu ya fedha za kigeni inatokana na misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka nje. **Mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi ni kidogo sana.** Ni lazima **tuweke nguvu mpya katika kukuza mauzo ya nje.**

**UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2004/05:**

21. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya maelezo kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu, napenda sasa kurejea katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2004/05. Kama alivyoeleza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, uchumi umekua kwa asilimia **6.7** mwaka 2004, mfumuko wa bei umeshuka kutoka asilimia **4.8** mwezi Machi 2004 hadi kufikia asilimia **4.1** mwezi Machi

2005, na unatarajiwa kufikia lengo la asilimia 4.0 mwisho wa Juni 2005. Akiba ya fedha za kigeni, hadi Machi 2005, ilikuwa inatosheleza kulipia mahitaji ya bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi cha miezi **8.3,** ikilinganishwa na lengo la miezi 6 ifikapo Juni 2005.

22. ***Mheshimiwa Spika***, katika bajeti ya mwaka 2004/05, Serikali ilidhamiria kupanua wigo wa kodi, na kuimarisha usimamizi na utawala wa Mamlaka ya Mapato, hasa kupanua Idara ya Walipakodi Wakubwa; kutekeleza Sheria mpya ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004; kufanya mapitio ya sheria mbalimbali za kodi, ikiwemo Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*), kwa lengo la kuziboresha. Aidha, Serikali ilitangaza hatua kadhaa za motisha ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya kilimo, na kurahisisha biashara kwa kurekebisha mfumo wa leseni za biashara na kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa bajeti ya 2004/05 hadi Machi 2005 unaonyesha matokeo ya kuridhisha. Ukusanyaji wa mapato umevuka lengo na matumizi yameendelea kuwa chini ya lengo, japo kwa kiasi kidogo zaidi ya miaka ya nyuma. Aidha, mikopo na misaada ya bajeti imepatikana kwa wakati kama ilivyotegemewa.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2004/05, Serikali ilipanga kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi 1,739,288 milioni sawa na asilimia 13.8 ya Pato la Taifa. Katika kipindi cha Julai 2004 hadi Machi 2005 mapato yalifikia Shilingi 1,314,524 milioni ambayo ni Shilingi 21,681 milioni au asilimia **2** zaidi ya makadirio ya Shilingi 1,285,257 milioni kwa kipindi hicho. Mwelekeo unaonyesha kuwa lengo la mapato kwa mwaka 2004/05 litafikiwa na kuvukwa kidogo. Matokeo ya hatua mbalimbali za kodi zilizochukuliwa mwaka 2004/05 pia ni ya kuridhisha.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** sehemu kubwa ya ongezeko la mapato imechangiwa na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi ya mapato. Ukusanyaji wa VAT uliongezeka kutokana na hatua ya kupandisha thamani ya Kampuni zinazotakiwa kujisajili kwa VAT kutoka shilingi milioni 20 kwa mwaka hadi shilingi milioni 40. Kwa maana nyingine, idadi ya walipa kodi ya VAT imepungua na hivyo kuongeza ufanisi katika ukusanyaji. Ongezeko la ukusanyaji wa kodi ya mapato limetokana na kodi ya ajira (PAYE) na kodi ya makampuni (corporation tax), kutokana na ufanisi wa ukusanyaji na kuziba mianya ya ukwepaji kodi, hasa katika kodi ya mapato, kwa sababu ya sheria mpya ya 2004. Sababu nyingine ni pamoja na kuanzisha kituo kimoja cha kulipia kodi za aina zote (one stop

centre) katika kila Wilaya; na pia kwa kupanua Idara ya Walipa Kodi Wakubwa ambayo imeboresha huduma kwa walipa kodi. Aidha, matumizi ya teknolojia ya kisasa pamoja na mafunzo kwa watoza kodi vimerahisisha ukusanyaji.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Ushuru wa Forodha, makusanyo halisi hayakufikia lengo kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi (Non-tax-revenue) ikijumuisha mapato yanayokusanywa na Wizara, Idara na Mikoa yalivuka lengo.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Nchi nyingi Wahisani na mashirika ya fedha ya kimataifa yameitikia wito wa kutupatia misaada kuchangia harakati zetu za kukuza uchumi na kuondoa umasikini. Katika kipindi cha Julai, 2004 hadi Machi, 2005, misaada na mikopo kwa ajili ya bajeti ilifikia Shilingi 429,676 milioni ikiwa ni Shilingi 4,800 milioni au asilimia **1.1** tu chini ya makisio ya Shilingi 434,476 milioni katika kipindi hicho. Hali kadhalika, jumla ya Shilingi 719,817 milioni zilipatikana katika kipindi hicho kama misaada na mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kiasi hiki ni Shilingi 134,442 milioni au asilimia **23** zaidi ya makisio ya Shilingi 585,376 milioni katika kipindi hicho.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2004 hadi Machi 2005, Serikali ilipanga kupunguza akiba yake kutoka Benki Kuu kwa Shilingi 118.200 milioni ili kugharamia matumizi yaliyopangwa. Hata hivyo, kutokana na ukusanyaji mzuri wa mapato ya ndani, Serikali haikupunguza akiba yake na badala yake akiba iliongezeka kwa Shilingi 81,368 milioni.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi 2005, matumizi yalifikia jumla ya Shilingi 2,429,269 milioni ikilinganishwa na makisio ya Shilingi 2,486.892 milioni katika kipindi hicho. Shilingi 1.560,067 milioni ni matumizi ya kawaida na Shilingi 869,202 milioni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika matumizi ya kawaida, Shilingi 152,122 milioni zimetumika kulipia madeni. Mishahara kwa watumishi wa Serikali ilikuwa Shilingi 409,333 milioni ikilinganishwa na makisio ya Shilingi 413,369 milioni. Kadhalika, madai halali ya walimu na watumishi wengine wa Serikali yaliyohakikiwa yamelipwa kama ilivyopangwa. Ili kudhibiti malimbikizo ya madai kama haya, utaratibu wa kuzuia malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa Serikali, wakiwemo walimu, unaimarishwa, kama ulivyofafanuliwa katika Waraka wa Hazina Na. 12 wa Mwaka 2004 uliosambazwa kwa Maafisa Wahasibu wote.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha na mali za umma. Serikali imetunga Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 ili kupanua madaraka na uwajibikaji ndani ya sekta ya umma. Utaratibu wa kutumia tulichonacho *"Cash Budget"* umeendelea kutumika katika kusimamia na kudhibiti matumizi ya Serikali. Mtandao wa kompyuta wa kusimamia malipo (*IFMS*) umeendelea kuimarishwa kwa kufunga vifaa vya tahadhari pindi mtandao uliopo ukipata matatizo (*disaster recovery site*). Mtandao huo unahakikisha kwamba, matumizi yanazingatia bajeti iliyopitishwa na Bunge na kwamba, ubadhirifu unabainishwa kwa haraka na kwa uhakika zaidi kuliko ilivyokuwa kabla ya mtandao huo. Baada ya kuunganisha Maafisa Wahasibu wote wa Wizara na Idara zinazojitegemea, hivi sasa mtandao umefikishwa katika Ofisi za Katibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara na pia katika Halmashauri 32 za Wilaya. Aidha, mafunzo kwa Wahasibu wa Serikali yanaendelea. Vile vile, Serikali imewarejesha wastaafu 10,813 waliokuwa wamechukua mafao yao kwa mkupuo katika Daftari la Pensheni.

## MWELEKEO WA BAJETI HADI JUNI, 2005

31. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia mwenendo wa bajeti wa mwaka wa fedha hadi mwezi Machi 2005, Serikali inaamini kwamba malengo ya mapato ya ndani, fedha za nje, na matumizi, yatafikiwa kama ilivyokadiriwa. Kwa upande wa matumizi, mwelekeo ni kwamba matumizi ya kawaida, hususan Matumizi Mengineyo (*OC*), hayatafikiwa kutokana na sababu zilizoelezwa awali. Hata hivyo, malengo ya matumizi katika sekta za kipaumbele za kukuza uchumi na kupunguza umaskini, yatafikiwa kama ilivyopangwa.

## MISINGI NA SHABAHA ZA BAJETI KWA MWAKA 2005/06

32. ***Mheshimiwa Spika,*** mfumo wa Bajeti ya mwaka 2005/06 unazingatia utekelezaji wa MKUKUTA. Malengo muhimu ya uchumi ni pamoja na:-

(i) Pato halisi la Taifa linalengwa kukua kwa asilimia **6.9** mwaka 2005, asilimia **7.2** mwaka 2006, asilimia **7.6** mwaka 2007, na asilimia **7.9** mwaka 2008;

(ii) Kasi ya upandaji bei itabakia **4** hadi Juni 2005 na baadaye kulingana na

viwango vya wastani katika nchi tunazofanya nazo biashara;

(iii) Uwiano kati ya mapato ya Serikali na Pato la Taifa (*revenue/gdp ratio*) utakuwa asilimia **14.3** mwaka 2005/06, asilimia **14.5** mwaka 2006/07 na asilimia **14.6** mwaka 2007/08;

(iv) Akiba ya fedha za kigeni itatosheleza mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 7; na

(v) Ongezeko la ujazi wa fedha (kwa tafsiri pana, $M_3$) litawiana na malengo ya ukuaji wa uchumi, na kasi ya upandaji bei nchini.

**Sera za Mapato**

33. ***Mheshimiwa Spika,*** sera za mapato kwa mwaka 2005/06, zinalenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua Shilingi **2,066,751** milioni (trilioni 2.067) sawa na asilimia **14.3** ya Pato la Taifa ikilinganishwa na mapato ya asilimia 13.8 mwaka 2004/05. Lengo hili la mapato ni ongezeko la asilimia **18.7** kwa mwaka 2005/06, ikilinganishwa na ongezeko la asilimia **20.7** linalotarajiwa mwaka 2004/05. Ili

kuendelea kuboresha ukusanyaji, hatua zifuatazo zitatekelezwa:

(i) Kuimarisha utendaji na usimamizi katika Idara ya Forodha.
(ii) Kurekebisha Muundo wa Mamlaka ya Mapato ili kuboresha zaidi usimamizi wa vianzo vya ndani.
(iii) Kuimarisha Idara ya Walipakodi Wakubwa, ili ihudumie walipakodi wengi zaidi;
(iv) Kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi katika maeneo kadhaa ili kurahisisha utekelezaji na ufanisi wa utawala wa kodi.
(v) Kuimarisha ukusanyaji na taarifa za mapato kutoka Wizara na Idara mbalimbali, hasa zile zilizo kwenye utaratibu wa *'Retention'*.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kukua kwa uchumi na kupanuka kwa wigo wa kodi, mageuzi makubwa yanayoendelea ndani ya Mamlaka ya Mapato chini ya Mpango wake wa Pili wa Miaka Mitano (*Second Corporate Plan*) yamekuwa chanzo muhimu cha kukua kwa mapato ya ndani. Katika mwaka wa 2005/06, Serikali itaendelea kuimarisha Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa kuboresha mifumo ya utendaji na taaluma na **kuhamishia huko makampuni yote ya madini ili kuboresha**

**mawasiliano na kampuni hizo.** Aidha, tutaendelea kuboresha usimamizi na utendaji katika Idara ya Forodha kwa kuongeza uwajibikaji, matumizi ya teknolojia, na kupunguza mlolongo wa taratibu ndefu. Katika zoezi hili, Serikali inashirikiana na Kituo cha Ushauri wa Utaalam cha IMF (East-AFRITAC), Shirika la Forodha la Kimataifa (WCO), na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo *(UNCTAD)*.

**Misaada na Mikopo ya Nje**

35. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza awali, kwa kutumia Mkakati wa Kusimamia Misaada (*Tanzania Assistance Strategy*) na ule wa Madeni (*National Debt Strategy*), Serikali imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na nchi wahisani pamoja na Mashirika ya Fedha ya Kimataifa. Misaada na mikopo ya masharti nafuu ya nje itachangia takribani asilimia 41 ya bajeti ya 2005/06. Pamoja na nia yetu ya kutaka kujitegemea, bado tunahitaji misaada ya nje ili itusaidie kujenga uwezo wa kujitegemea hatua kwa hatua katika kipindi kijacho, pamoja na kusaidia kutekeleza kwa haraka mikakati ya kufikia malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs). Tutaendelea kushauriana na nchi wafadhili kwa lengo la kuongeza misaada ya bajeti.

**Vianzio vingine vya mapato**

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2005/06 Serikali inakusudia kuuza hisa zake zenye thamani ya Shilingi 10,420 milioni katika baadhi ya kampuni na mashirika, na kutumia akiba yake katika Benki Kuu ya Tanzania kwa kiasi cha shilingi 259,225 milioni. Papo hapo, Serikali inaangalia upya sera ya kuuza hisa katika mashirika yenye faida na maslahi mengine ya kitaifa, kwa lengo la kutouza hisa zake zote kwenye kila shirika.

**Sera za Matumizi**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2005/06, Serikali itaendelea kuimarisha nidhamu katika matumizi ya fedha za umma na kuhakiki uwajibikaji. Aidha, utaratibu wa kutumia tulicho nacho (cash budget) utaendelea katika mwaka ujao ili kuhakikisha kwamba Serikali inaishi ndani ya uwezo wake. Vile vile, uwezo wa Ukaguzi wa Ndani katika Wizara na Idara za Serikali utaimarishwa kwa kuendelea kutoa mafunzo ili kuwezesha Wakaguzi wa ndani kufuatilia vyema hoja za ukaguzi na kutoa ushauri nasaha kwa maafisa wahasibu. Mafunzo kuhusu taratibu za uhasibu na ukaguzi wa ndani yataendelezwa na kuimarishwa. Serikali inatarajia kupanua mtandao wa malipo kwa kompyuta kwenye Halmashauri zingine 32 za

Wilaya katika mwaka ujao wa fedha. Hatua hii inategemewa kuboresha usimamizi wa matumizi katika Halmashauri hizo kwa kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwa haraka.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupanga mgao wa fedha za bajeti kwa mwaka wa fedha 2005/06, mambo yafuatavyo yamezingatiwa:

(i) Asilimia zaidi ya 50 ya bajeti ya 2005/06 imetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa katika MKUKUTA ambavyo ni:-
- kukuza uchumi na kuondoa umaskini wa kipato,
- kuimarisha hali za maisha na hifadhi ya jamii, na
- kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

(ii) Aidha, kiasi kikubwa cha fedha kimetengwa kwa ajili ya sekta za huduma za uchumi na huduma za jamii ili kulinda mafanikio yaliyopatikana chini ya Mkakati wa awali wa Kupunguza Umaskini (PRSP). Sekta zinazoongoza kwa kutengewa hizo fedha nyingi ni pamoja na Ujenzi, Afya, Elimu, Kilimo na Maji

(iii) Fedha za kutosha zimetengwa kwa ajili ya gharama zilizobaki za Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba 2005.

(iv) Bajeti hii pia imetenga asilimia **4.5** ya misaada ya bajeti kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(v) Bajeti hii imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa madawa ya kusaidia kurefusha maisha kwa waathirika wa ugonjwa wa ukimwi pamoja na kupiga vita malaria na kifua kikuu.

(vi) Bajeti ya 2005/06 imetenga fedha za malipo ya mafao ya waliokuwa watumishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(vii) Kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo, bajeti ya mwaka 2005/06 imetenga fedha kwa ajili ya mahitaji hayo. Aidha, majadiliano yanaendelea yanayohusisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuongeza vyumba vya madarasa, mabweni, maabara n.k. katika Vyuo vya Elimu ya Juu.

(viii) Serikali imeamua kutenga moja ya nane (⅛) ya Ada ya Ufundi Stadi (Skills Development Levy) kwa ajili ya Mfuko wa Elimu (Tanzania Education Fund) ili kuongeza kasi ya kupanua miundo mbinu ya elimu nchini.

(ix) Bajeti imetenga fedha kwa ajili ya mishahara ya watendaji wote wa Vijiji, ikiwemo ile ambayo haikulipwa kama bado ipo. Hii ni Awamu ya Pili ya mpango huo. Awamu ya Kwanza imetekelezwa mwaka huu wa 2004/05 na ilihusisha watumishi **7,770.**

(x) Katika bajeti ya 2005/06, Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) zitapatiwa **mapato yote** yatokanayo na Ada ya Viwanja vya Ndege (Passenger Service Charge), badala ya asilimia 90 ya sasa, ili kuhimili gharama kubwa za kuendesha viwanja vya ndege.

(xi) Juhudi za kuimarisha utawala bora zimezingatiwa. Fedha zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji

wa Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa katika bajeti za Wizara zote, na pia kupitia bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, kwa ajili ya kuboresha utendaji wa mfumo wa Mahakama nchini.

(xii) Bajeti hii imetenga **asilimia 18** ya mapato ya ndani kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**MFUMO WA BAJETI YA MWAKA 2005/06:**

39. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza awali, Serikali inalenga kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya Shilingi **2,066,751** milioni katika mwaka wa fedha 2005/06. Kiwango hiki cha mapato ni asilimia **14.3** ya Pato la Taifa. Serikali inategemea pia kupata shilingi 10,424 milioni kutokana na ubinafsishaji.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa matumizi, katika mwaka 2005/06 Serikali imepanga kutumia jumla ya Shilingi **4,176,050** milioni. Misaada na Mikopo ya nje (ikijumuisha misamaha ya madeni) itakuwa Shilingi **1,724,910** milioni. Kati ya fedha hizi, Shilingi **616,165** milioni ni misaada na mikopo ya kusaidia bajeti moja kwa moja; na Shilingi **93,600** milioni ni misamaha ya madeni, wakati Shilingi **1,015,145** milioni ni mikopo na

misaada kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kama nilivyoeleza hapo awali, Serikali inakusudia kuuza hatifungani maalum kwenye soko **kwa ajili ya miundombinu.** Aidha, shilingi **259,225** milioni zitapatikana kwa kupunguza akiba ya Serikali katika Benki Kuu.

## MAREKEBISHO YA MFUMO WA KODI, ADA MBALIMBALI NA HATUA NYINGINE ZA MAPATO

41. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza jitihada za kuboresha mfumo wa kodi na taratibu za ukusanyaji mapato, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika maeneo yafuatayo:

(a) Sheria ya Kodi ya Mapato
(b) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani
(c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa
(d) Ada ya leseni za magari
(e) Ada ya Leseni za Usafirishaji
(f) Sheria ya Ushuru wa Stempu
(g) Sheria ya Mfuko wa Elimu

**Sheria ya Kodi ya Mapato**

42. ***Mheshimiwa Spika***, Inapendekezwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 ili kuongeza kiwango cha chini cha mapato ya ajira yasiyotozwa kodi,

kutoka shilingi 60,000 kwa mwezi hadi shilingi 80,000 kwa mwezi. Hatua hii ina lengo la kuwaondoa kwenye wigo wa kodi wafanyakazi wa kipato cha chini na kutoa unafuu wa kodi kwa wafanyakazi hao kama njia ya kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA). Viwango vya sasa na vinavyopendekezwa vimeonyeshwa katika jedwali namba 1. Viwango vya ukokotoaji wa kodi hiyo vimebaki kama ilivyokuwa kwa ngazi mbalimbali za mishahara, yaani asilimia 18.5, 20,25, na 30.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Marekebisho haya yatapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shillingi 27,970 milioni. Hata hivyo, nyongeza ya mishahara ya watumishi pamoja na ufanisi katika usimamizi wa kodi vinatarajiwa kuongeza mapato na hivyo kupunguza pengo hadi ***shilingi 1,822 milioni.***

**SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI (VAT)**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika eneo hili:-

(i) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Tatu la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuingiza kwenye msamaha huo vipuri vya

treni na vifaa vingine vinavyotumika katika treni. Marekebisho haya yatasaidia kupunguza gharama za usafirishaji na kusaidia TRC na TAZARA kumudu gharama za matengenezo.

(ii) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Pili la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuingiza kwenye msamaha huo mafuta ya ndege kwa wenye ndege za kibiashara au huduma za jamii za hapa nchini. Hatua hii inalenga kuwawezesha wenye ndege hizo hapa nchini kuhimili ongezeko kubwa la gharama za kuendeshea ndege, hasa baada ya balaa la Septemba 11, na ongezeko la sasa la bei ya mafuta ya ndege. Hatua hii italinda utalii na ndege zinazohudumia wagonjwa, kilimo, hifadhi, viongozi, Polisi, Jeshi n.k.

(iii) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Tatu la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili kuingiza kwenye msamaha wa VAT magari yanayotumika kutoa huduma za afya (Mobile Health Clinic) ili kuvutia huduma hizo katika maeneo yasiyo na vituo vya afya au zahanati.

(iv) Kufanya marekebisho katika Jedwali la Tatu la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kuondoa kifungu cha sasa kinachotoa msamaha wa kodi kwa shughuli za uchimbaji madini kwa vile msamaha kama huo umetolewa kwenye vifungu vingine vya sheria hiyo.

Hatua hizi katika kodi ya VAT kwa ujumla zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi **2,685 milioni.**

**Sheria ya Ushuru wa Bidhaa:**

45. ***Mheshimiwa Spika***, inapendekezwa kufanya marekebisho yafuatayo katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa:

*(a)* ***Mafuta ya Ndege***

Inapendekezwa kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya ndege (Jet A-1) ili kuwepo usawa katika ushindani kwa faida ya kampuni za ndege za hapa nchini.

*(b)* ***Viwango vya Ushuru wa Bidhaa***

46. ***Mheshimiwa Spika***, inapendekezwa kurekebisha viwango vya Ushuru wa Bidhaa

kwa asilimia **tano tu**, sawa na mfumuko wa bei, kwa bidhaa zifuatazo:-

(i) Vinywaji baridi kutoka shilingi 39.4 kwa lita hadi shilingi 41.5 kwa lita;

(ii) Bia kutoka shilingi 243 kwa lita hadi shilingi 256 kwa lita;

(iii) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka shilingi 780 kwa lita hadi shilingi 820 kwa lita;

(iv) Vinywaji vikali kutoka shilingi 1,158 kwa lita hadi shilingi 1,216 kwa lita;

(v) Kurekebisha mfumo wa kutoza Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara ili kutumia kigezo cha kuwa na kichungi (filter) badala ya urefu wa sigara pamoja na kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kama ifuatavyo:

(a) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 3,970 hadi shilingi 4,170 kwa sigara elfu moja;

(b) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi 9,367 hadi shilingi 9,840 kwa sigara elfu moja;

(c) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 17,017 hadi shilingi 17,870 kwa sigara elfu moja;

(d) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara ("cut filler") kutoka Shilingi 8,593 hadi shilingi 9,025 kwa kilo;

(e) Ushuru wa Bidhaa kwa "Cigar" unabaki kuwa asilimia 30.

Marekebisho haya ya ushuru wa bidhaa kwa pamoja yanatarajiwa kuipatia Serikali mapato mapya ya kiasi cha ***shilingi 4,418.6 milioni.***

**Ada ya Leseni za Magari na Usafirishaji zinazokusanywa na Mamlaka mbalimbali:-**

47. ***Mheshimiwa Spika***, katika eneo hili, inapendekezwa kufanya marekebisho ya viwango vya baadhi ya ada zinazotozwa na vyombo mbalimbali. Lengo ni kuondoa kero,

kuboresha mazingira ya biashara, na kufidia gharama za usajili wa magari.

(i) Kufuta ada za leseni za usafirishaji zinazotozwa na mamlaka mbalimbali za leseni za usafirishaji, kwa magari yasiyochukua abiria ikiwa ni pamoja na pick-ups na magari makubwa ya mizigo;

(ii) Asilimia 10 ya ada ya huduma kwa abiria wa ndege (Passenger Service Charge) ambayo inaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali sasa itapelekwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege;

(iii) Kuongeza kiwango cha Ada ya Gari kutoka shilingi 10,000.0 hadi shilingi 20,000.0 kwa gari kwa mwaka.

Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha s***hilingi 1,125 milioni***.

**Ushuru wa Stempu:**

48. ***Mheshimiwa Spika***, inapendekezwa kupunguza kiwango cha ushuru wa stempu kutoka asilimia nne (4%) hadi asilimia moja (1%) ya thamani ya mali husika kwenye maeneo yafuatayo:-

(a) Kubadilishana mali (exchange of property);
(b) Hati ya Mauzo (bill of sale);
(c) Cheti cha mauziano (certificate of sale);
(d) Hati ya Zawadi (instrument of gift);
(e) Uhamisho wa mali ya kukodi (Transfer of lease by way of assignment);
(f) Instrument of partition;
(g) Instrument of release;
(h) Instrument of settlement.

49. ***Mheshimiwa Spika***, inapendekezwa pia kupunguza kiwango cha Ushuru wa Stempu kwenye utambuzi wa madeni (acknowledgement of debt) kutoka asilimia 4 na kuwa Shilingi 500.

Hatua hizi zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha ***shillingi 1,996 milioni***.

**Sheria ya Mfuko wa Elimu**

50. ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na uamuzi wa Serikali wa kuupatia Mfuko wa Elimu moja ya nane ($^1/_8$) ya mapato yanayotokana na Ada ya Ufundi Stadi, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Mwaka 2001 ili kufuta vifungu vinavyotoa msamaha wa Kodi ya

Mapato, VAT na Ushuru wa Forodha kwa wanaochangia Mfuko huo. Hata hivyo, wachangiaji wataendelea kupata punguzo la kodi kwa mujibu wa kifungu cha 16 (1) (b) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004.

Hatua hii haiongezi wala kupunguza mapato ya Serikali.

**Marekebisho katika baadhi ya Sheria nyingine za Kodi**

51. ***Mheshimiwa Spika***, inapendekezwa kufanya marekebisho sheria mbalimbali za fedha na kodi ili ziendane na wakati na kurahisisha utekelezaji wake. Hatua hii haina athari kwa mapato ya Serikali.

**Sheria ya Misitu na Kanuni zake**

52. ***Mheshimiwa Spika***, inapendekezwa kufuta Ada ya Leseni ya Ukazi (License to reside in a forest reserve) na Ada ya Leseni ya Kulima kwenye msitu wa Serikali au kampuni (licence to cultivate in a forest reserve) wanazotozwa wananchi walioruhusiwa kuishi katika misitu ya hifadhi ili kuondoa kero kwa wananchi hao. Aidha, inapendekezwa kwamba leseni za kuendesha biashara katika misitu hiyo zikatwe mara moja tu kama ilivyorekebishwa kwa biashara nyinginezo mwaka jana.

Hatua hii haina athari yoyote kwa mapato ya Serikali, lakini inaondoa kero kwa wananchi wanaoishi katika msitu ya hifadhi.

**Sheria ya Ushuru wa Forodha**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** tangu tulipoanza kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwezi Januari 2005, tumepokea mapendekezo ya marekebisho ya viwango vya ushuru wa pamoja wa Forodha (EAC Common External Tariff) kutoka kwa wadau mbalimbali kupitia kamati maalumu ya kurekebisha mfumo wa kodi nchini. Serikali za Kenya na Uganda pia zilipokea mapendekezo kutoka kwa wadau wao.

Mapendekezo ya Tanzania pamoja na yale ya kutoka Kenya na Uganda yalijadiliwa katika kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Nchi Wanachama wa Jumuiya kilichofanyika Arusha tarehe 14 Mei 2005. Mapendekezo hayo ya Mawaziri wa Fedha yatawasilishwa kwenye kikao cha Kisekta cha Mawaziri wa Biashara, Fedha na Uwekezaji wa Nchi Wanachama wa Jumuiya, kitakachofanyika tarehe 20 Juni 2005, kama ilivyoagizwa na kikao cha Wakuu wa Nchi hizo kilichofanyika tarehe 29 - 30 Mei 2005. Marekebisho yatakayoidhinishwa yatatekelezwa pamoja na hatua nilizozielezea katika Hotuba hii.

**Muda wa Kodi Mpya Kutumika**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizi za kodi mpya na zile zitakazo idhinishwa na kikao cha Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki cha tarehe 20 Juni, 2005 zitaanza kutumika tarehe 1 Julai, 2005 isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo.

**Matokeo**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** marekebisho yanayopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

| | **Hatua** | **Shilingi Milioni** |
|---|---|---|
| (i) | Kodi ya Mapato inayotokana na ajira | (1,822) |
| (ii) | Ushuru wa Stempu | (1,996) |
| (iii) | Kodi ya Ongezeko la Thamani | (2,685) |
| (iv) | Ushuru wa Bidhaa | 4,419 |
| (v) | Ada za Leseni | 2,084 |
| | **JUMLA** | **0** |

56. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia mfumo wa bajeti niliouelezea hapo juu, sura ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2005/06 inakuwa kama ilivyo kwenye **jedwali namba 2.**

57. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muhtasari, bajeti ya mwaka 2005/06 itagharimu shilingi

**trilioni 4, bilioni 176, milioni 50** (4,176,050 milioni).

(a) Mapato ya ndani kutokana na kodi, yasiyo ya kodi na mapya yanategemewa kufikia shilingi **trilioni 2, bilioni 66 milioni 752** (2,066,752 millioni).

(b) Mapato kutokana na misaada na mikopo, akiba toka Benki Kuu ya Tanzania, mauzo ya hisa za mashirika, na mikopo ya ndani isiyo ya kibenki yanatarajiwa kufikia shilingi **trilioni 2, bilioni 109, milioni 298** (2,109,298 milioni).

Kwa upande wa matumizi ya kawaida, Serikali inatarajia yatafika shilingi **trilioni 2, bilioni 790, milioni 867** (2,790,867 milioni). Gharama hizo ni kwa ajili ya Deni la Taifa, Wizara, Mikoa, Halmashauri, mishahara ya watumishi katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Taasisi, pensheni, na dharura.

Matumizi ya maendeleo yatatokana na fedha za ndani shilingi **bilioni 370 na za nje shilingi trilioni moja, bilioni 15 milioni 145** (1,015,145 milioni), **jumla trilioni moja, bilioni 385, milioni 183** (1,385,183 milioni).

Jumla ya Mapato na Matumizi inawiana, yaani shilingi **trilioni 4, bilioni 176, milioni 50** (4,176,050 milioni).

**Mwisho**

58. ***Mheshimiwa Spika***, kazi iliyofanyika katika kipindi hiki cha Awamu ya Tatu ni kubwa, na Watanzania wote tunayo haki ya kujipongeza. Lakini naamini tutakuwa wachoyo wa shukrani kama hatutatambua mchango mkubwa na wa kipekee wa Jemadari wetu katika vita hii, Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, Rais wetu na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Mheshimiwa Rais Mkapa amekuwa Kiongozi asiyeyumbishwa katika kulinda maslahi ya Taifa wakati wa kutekeleza mageuzi yaliyotuletea mapinduzi tunayojivunia sasa. Hakuyumba wakati baadhi yetu tulipokuwa tukipiga kelele za "ukapa", ukata, kuuza nchi, n.k. Amedhihirisha uelewa mkubwa wa uchumi wetu na wa duniani, ameonyesha ubunifu wa hali ya juu sana katika kupanga sera na mikakati mbalimbali iliyozaa matunda haya, na amekuwa msimamizi hodari wa utekelezaji na ufuatiliaji wa mikakati iliyoamuliwa. Aidha, ushiriki wake katika majukumu ya ndani na hata ya kimataifa hata alipo kuwa mgonjwa, umesaidia sana kuijengea nchi yetu heshima na kuvutia wawekezaji na wahisani. Nchi yetu imekuwa na bahati kubwa kumpata Mheshimiwa Mkapa kama kiongozi wetu Mkuu wakati huo na katika kipindi hiki muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. Ni imani yangu kuwa, endapo dalili zinazojitokeza kuashiria

kuwa Serikali ijayo ya Chama cha Mapinduzi itafuata nyayo za Rais Mkapa zitatimia, matumaini ya wananchi ya kuboresha zaidi uchumi na kuutokomeza umaskini kwa "nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya" yataifanya Tanzania izidi kumeremeta na kupaa. Binafsi naona fahari kubwa na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa katika timu inayojiandaa kuipisha timu mpya Serikalini baada ya kufunga magoli mengi ilipokuwa uwanjani.

59. ***Mheshimiwa Spika***, bajeti ya mwaka 2005/06 imeandaliwa kuwa daraja la kuendeleza juhudi za Serikali katika:-

(i) Kuhitimisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama Tawala mwaka 2000 na kuanza Ilani ya mwaka 2005 bila kuzubaa zubaa.

(ii) Kuweka misingi ya utekelezaji wa sera za Chama Tawala chini ya Serikali ya Awamu ya Nne;

(iii) Kuendelea kuhimiza utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa hadi 2025;

(iv) Kuanza kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania - MKUKUTA;

(v) Kutekeleza Sera za Kijumla za Kiuchumi kwa mwaka 2005/06.

60. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa malengo na mikakati niliyoitaja hapo juu inategemea juhudi za dhati za kila Mtanzania, kila mzalendo na kila mwenye nia njema na taifa letu, ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na huduma za jamii. Lengo letu kubwa ni kuhakikisha umaskini unapungua haraka, hatua kwa hatua. Kama nilivyoeleza hapo awali, uchumi wetu unaendelea kukua kwa kiwango cha kuridhisha. Hata hivyo, kwa kasi ya ongezeko la watu la karibu asilimia 3 kwa mwaka, itachukua **si chini ya miaka 20 kuongeza maradufu pato la wastani la wananchi** (*income per capita*) tukiweza kufikia kasi ya kukua kwa uchumi ya asilimia 8 kwa mwaka. Tukizingatia kwamba pato jipya la wastani bado litakuwa chini ya Dola 2 za Kimarekani kwa siku, ni dhahiri kwamba tutakuwa bado hatujapiga hatua kubwa, hata tukipata mafanikio hayo. Kwa hiyo, tunahitaji kuwa wabunifu zaidi na pia kung'ang'ania kusukuma maeneo muhimu katika uchumi, ili kupata njia mpya za kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi na kufikia zaidi ya asilimia 10 kwa mwaka.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** bajeti hii inapendekeza kuanza kuchukua hatua katika eneo la miundombinu ya aina aina ambayo imeonekana kuwa ni kikwazo kikubwa kwa juhudi zetu za kukuza uchumi. Katika Awamu inayokuja, mikakati zaidi inahitajika ili kuimarisha na kuendeleza changamoto hii.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

*Jedwali Na. 1*

**VIWANGO VYA KODI YA MAPATO YA AJIRA (PAYE)**

**Viwango vya Sasa**

| **Mapato kwa mwezi** | **Kodi kwa Mwezi** |
|---|---|
| Shilingi 0 mpaka Shilingi 60,000 | Hakuna kodi |
| Shilingi 60,001 mpaka Shilingi 180,000 | Asilimia 18.5 ya mapato yanayozidi Shilingi 60,000 |
| Shilingi 180,001 mpaka Shilingi 360,000 | Shilingi 22,200 na kuongeza asilimia 20 ya mapato yanayozidi Shilingi 180,000 |
| Shilingi 360,001 mpaka Shilingi 540,000 | Shilingi 58,200 na kuongeza asilimia 25 ya mapato yanayozidi Shilingi 360,000 |
| Zaidi ya Shilingi 540,000 | Shilingi 103,200 na kuongeza asilimia 30 ya mapato yanayozidi Shilingi 540,000 |

**Viwango Vinavyopendekezwa**

| **Mapato kwa mwezi** | **Kodi kwa Mwezi** |
|---|---|
| Shilingi 0 mpaka Shilingi 80,000 | Hakuna kodi |
| Shilingi 80,001 mpaka Shilingi 180,000 | Asilimia 18.5 ya mapato yanayozidi Shilingi 80,000 |
| Shilingi 180,001 mpaka Shilingi 360,000 | Shilingi 18,500 na kuongeza asilimia 20 ya mapato yanayozidi Shilingi 180,000 |
| Shilingi 360,001 mpaka Shilingi 540,000 | Shilingi 54,500 kuongeza asilimia 25 ya mapato yanayozidi Shilingi 360,000 |
| Zaidi ya Shilingi 540,000 | Shilingi 99,500 kuongeza asilimia 30 ya mapato yanayozidi Shilingi 540,000 |

**Sura ya Bajeti 2005/06**

| | Mapato | | | Shilingi Milioni |
|---|---|---|---|---|
| A: | **Mapato ya Ndani** | | | **2,066,751** |
| | *(i) Mapato ya Kodi* | | | 1,897,506 |
| | *(ii) Mapato yasiyo ya Kodi* | | | 169,245 |
| | *(iii) Mapato Mapya* | | | |
| B: | Mikopo na Misaada ya Nje (*Ikiju muisha HIPC*) | | | 1,724,910 |
| C: | Kupunguza akiba (*Draw Down of Reserves*) | | | 259,225 |
| D: | Mapato kutokana na mauzo ya hisa | | | 10,420 |
| E: | Mikopo isiyo ya Benki | | | 114,744 |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE** | | | **4,176,050** |
| F: | Matumizi ya Kawaida | | | 2,790,867 |
| | *(ii) Deni la Taifa* | | 528,144 | |
| | *(iii) Wizara* | | 1,617,178 | |
| | *(iv) Mikoa* | | 37,790 | |
| | *(v) Halmashauri* | | 484,150 | |
| | *(vi) Matumizi Maalum* | | 123,605 | |
| | • *Marekebisho ya Mishahara Serikali Kuu na Serikali za Mitaa* | 80,731 | | |
| | • *Marekebisho ya Mishahara Mashirika* | 10,000 | | |
| | • *Retrenchment* | 1,500 | | |
| | • *Mchango wa Serikali Pensheni* | 12,024 | | |
| | • *Dharura* | 19,350 | | |
| G: | Matumizi ya Maendeleo | | | 1,385,183 |
| | *(i) Fedha za Ndani* | | 370,038 | |
| | *(ii) Fedha za Nje* | | 1,015,145 | |
| | **JUMLA YA MATUMIZI YOTE** | | | **4,176,050** |

**Jedwali No. 3: Kiwango cha Mikopo Mipya ya Ndani na Nje (Bilioni Shilingi)**


| | 2004/05 | 2005/06 |
|---|---|---|
| **1. Jumla ya Mikopo ya Ndani na Nje (a+b)** | 1,056.8 | 1293.3 |
| **(a) Mikopo Mipya ya Ndani** | 497.6 | 579.7 |
| (i) Dhamana za Serikali za muda mfupi | 296.0 | 335.2 |
| (ii) Hatifungani za Serikali | 201.6 | 244.5 |
| | | |
| **(b) Mikopo Mipya ya Nje (disbursements)** | 559.2 | 713.6 |
| (i) Miradi ya maendeleo | 390.9 | 442.9 |
| (ii) Bajeti | 168.3 | 270.7 |
| | | |
| **(c) Malipo ya Madeni ya Ndani** | 497.6 | 465.0 |
| (i) Dhamana za Serikali za muda mfupi | 296.0 | 335.2 |
| (ii) Hatifungani za Serikali | 201.6 | 129.8 |
| (iii) Riba | 94.9 | 83.1 |
| **(d) Malipo ya Madeni ya Nje** | 206.9 | 203.3 |
| (i) Riba | 73.5 | 74.6 |
| (ii) Mtaji | 133.4 | 128.7 |
| **(e) Ongezeko halisi la mikopo ya Ndani (a-c)** | - | 114.7 |
| **(f) Ongezeko halisi mikopo ya nje** | 425.8 | 584.9 |
| | | |
| **2. Ongezeko halisi la mikopo ya ndani na Nje (d+e)** | 425.8 | 699.6 |

| **Viashiria Muhimu vya Madeni** | [illegible] | [illegible] 2006 |
|---|---|---|
| Deni la Ndani / Jumla ya mikopo yote | 20.6% | 20.1% |
| Deni la Nje / Jumla ya mikopo yote | 79.4% | 79.9% |
| Jumla ya Deni / Pato la Taifa | 69.3% | 62.9% |
| **Jumla ya Deni / Mapato ya Ndani** | 491.1% | 440.1% |
| Malipo Nje/Mauzo ya Nje | 15.7% | 15.5% |
| **Malipo ya deni / Mapato ya Ndani** | 17.4% | 13.9% |
| | | |
| $GDP_{mp}$ | 12,567.1 | 14,457.90 |


Chanzo: Wizara Ya Fedha

**Jedwali na. 4: Deni la Tanzania na Mwenendo Wake kwa Mwaka wa Fedha 2005/06 (Sh. Bilioni)**


| | [illegible] | [illegible] |
|---|---|---|
| Jumla ya Deni la Taifa | 8,714.6 | 9,091.9 |
| Serikali Kuu | 7275.1 | 7,683.7 |
| Sekta nyingine za Umma | 1105.4 | 1,051.9 |
| Sekta Binafsi | 333.0 | 356.3 |
| Deni la Ndani | 1791.4 | 1,831.4 |
| Serikali Kuu | 1073.4 | 1,113.4 |
| Sekta nyingine za Umma | 718.0 | 718.0 |
| Deni la Nje | 6923.2 | 7,260.5 |
| Serikali Kuu | 6,201.7 | 6,570.3 |
| Sekta nyingine za Umma | 388.4 | 333.9 |
| Sekta Binafsi | 333.0 | 356.3 |
| **Mwenendo wa Deni la Taifa** | **2004/05** | **2005/06** |
| 1.0 Malipo ya Deni | 659.7 | 728.6 |
| Ndani | 462.8 | 525.3 |
| Nje | 206.9 | 203.3 |
| 1.1 Malipo ya Mikopo (principal repayment) | 491.3 | 553.8 |
| Ndani | 357.9 | 425.1 |
| Nje | 133.4 | 128.7 |
| 1.2 Malipo ya Riba (interest repayment) | 168.4 | 174.8 |
| Ndani | 94.9 | 100.2 |
| Nje | 73.5 | 74.6 |
| 2.0 Jumla ya Mikopo | 961.4 | 1,178.7 |
| Ndani | 402.2 | 465.1 |
| Dhamana za Serikali za muda mfupi | 335.1 | 335.3 |
| Hatifungani za Serikali | 67.1 | 129.8 |
| Nje | 559.2 | 713.6 |
| Miradi ya Maendeleo | 390.9 | 442.9 |
| Bajeti | 168.3 | 270.7 |
| 3.0 Misaada toka Nje | 807.9 | 1011.4 |
| Miradi ya Maendeleo | 467.0 | 572.3 |
| Bajeti (PRBS) | 266.2 | 346.5 |
| Msamaha wa madeni wa HIPC: | 74.7 | 93.6 |
| IDA | | |
| IMF | | |
| ADB/F | | |
| *Thamani halisi bidhaa zilizoagizwa Nje | | |
| Na | | |
| Wastani wa kiwango cha ubadilishaji fedha kwa kipindi chote (TZS/USD) | 1,121.0 | 1,080.0 |
| NB: | | |
| Ukuaji wa Pato halisi la Taifa (Real GDP) (kwa mwaka unaoishia) | 6.0% | 5.9% |
| Mfumuko wa bei (kwa mwaka unaoishia) | 4.0% | 4.0% |
| Bidhaa na huduma zilizoagizwa Nje | 1,315.6 | 1,315.6* |
| Pato la Taifa katika bei ya sasa ya soko (GDP m.p.) | 12,567.8 | 14,457.9 |
| Jumla ya Mapato ya Ndani (kwa mwaka unaoishia) | 1,739.3 | 2,065.7 |





Chanzo: Benki Kuu





Chanzo: Idara ya Taifa ya Takwimu





Chanzo: Wizara ya Fedha





Chanzo: Wizara ya Fedha




Chanzo: Wizara ya Fedha




Chanzo: Wizara ya Fedha na Benki Kuu




Chanzo: Benki Kuu

